HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

TAARIFA YA MGOGORO WA ARDHI KATIKA VIJIJI VYA KIBAKWE NA IYENGE

1: 0 UTANGULIZI

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ilipokea malalamiko ya wananchi wanne kutoka katika kijiji cha Kibakwe wakilalamika kuwa Serikali ya Kijiji cha Kibakwe na Kijiji cha Iyenge inawazuia kulima katika mashamba yao ambayo wamekuwa wakilima kwa muda mrefu. Aidha mgogoro huu uliwasilishwa na walalamikaji katika ofisi ya Mh. Mkuu wa Wilaya mwezi Desemba, 2017 na hatimaye ofisi hiyo iliiagiza Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya kushughulikia mgogoro huo. Baada ya Ofisi ya Mkurugenzi kupokea mgogoro huu kutoka kwa walalamikaji na kupokea maelekezo ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, kikosi kazi cha kushughulikia migogoro ya ardhi ya Wilaya na watalaam wa Idara ya ardhi walielekezwa kushughulikia mgogoro huu.

2:0 CHANZO CHA MGOGORO

Kutokana na maelezo ya pande husika na mazingira ya eneo la mgogoro, chanzo cha mgogoro huu kinatokana na mvutano wa miliki na matumizi ya ardhi iliyopo ndani ya mipaka ya kijiji cha Iyenge. Kwa upande mmoja ardhi hiyo ipo katika mipaka ya kijiji cha Iyenge na kwa upande mwingine wananchi wanaotumia ardhi hiyo ni wakazi wa kijiji cha Kibakwe. Wananchi wanne wa kijiji cha Kibakwe ambao ni ndugu Mchiwa Bakari, Geophrey Chuguru, Selina Mbiduka na Damiani Mbiduka wanadai kuwa Serikali za vijiji vya Kibakwe na Iyenge zinawazuia wasilime maeneo yao kwa madai kuwa eneo hilo lilikuwa ni shamba la kijiji, eneo la hifadhi HADO na baadaye eneo la ujenzi wa Chuo cha VETA.

3:0 JITIHADA ZA UTATUZI

Baada ya mgogoro huu kupokelewa, mnamo tarehe 20/01/2018 Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ilituma watalaam wa Idara ya Ardhi na wajumbe wa kikosi cha kushughulikia migogoro kufika

katika kijiji cha Kibakwe na kuzikutanisha pande husika na mgogoro huo. Pia wajumbe wa Serikali ya kijiji cha Iyenge, viongozi na watalaam wa Kata ya Kibakwe na Afisa Tarafa wa Kibakwe walishirikishwa.

4:0 KIKAO CHA UTATUZI

Kikao cha utatuzi kilifanyika katika ofisi ya Mtendaji wa Kijiji cha Kibakwe, baada ya pande husika kukutanishwa, watalaam kutoka Wilayani walieleza kwa kifupi maudhui ya kikao hicho na hatimaye pande husika kupewa nafasi ya kutoa maelezo yao. Kwa hatua ya awali, walalamikaji ndio walianza kutoa maelezo ya malalamiko yao kama ifuatavyo;

4.1 Mlalamikaji wa 1 ndugu Mchiwa Bakari

Mwananchi huyu alieleza kuwa, mwezi Desemba yeye na wenzake waliambatana kwenda katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwenda kutoa taarifa juu ya mgogoro uliojitokeza baina yao na viongozi wa vijiji vya Kibakwe na Iyenge. Aliendelea kueleza kuwa mnamo mwezi Desemba, 2016 walipewa taarifa na Mtendaji wa kijjiji vha Kibakwe, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kibakwe, Mtendaji wa Kata ya Kibakwe na Diwani wa Kata ya Kibakwe kuwa wasiendelee kulima mashamba yao kwa madai kuwa tumevamia eneo la ujenzi wa chuo cha VETA.

Pia ilielezwa kuwa; baadhi ya wananchi waliamua kulima bila kujali katazo walilopewa, mnamo tarehe 22/12/2016 wananchi wote waliokatazwa kulima eneo hilo waliitwa na kuelekezwa wafike kwenye mashamba yenye mgogoro ili waoneshwe yalivyochukuliwa. Baada ya kufika mashambani inaelezwa kuwa walioneshwa maeneo ya kutolima kwa vile ni sehemu ya maeneo ya HADO.

Baada ya kuona hakuna muafaka uliofikiwa katika eneo la mgogoro, mwananchi huyu anadai kuwa wao kama wamiliki wa mashamba yaliyochukuliwa na kijiji kwa matumizi ya ujenzi wa

chuo cha VETA waliamua kuwasilisha malalamiko yao kwa Afisa Tarafa wa Kibakwe ili atatue mgogoro huo kama ulivyokuwa umejitokeza. Baada ya malalamiko kuwasilishwa kwa Afisa Tarafa, kiongozi huyo aliomba ufafanuzi wa na maelezo ya mgogoro huu kutoka kwa Mtendaji wa Kata ya Kibakwe, Mtendaji huyo alitoa ufafanuzi kuwa wananchi wenye mgogoro walikubali kutoa maeneo hayo ili yatumike kwa ujenzi wa chuo cha VETA. Hatimaye Afisa Tarafa alitoa maelekezo kuwa malalamiko ya wananchi hao yawasilishwe kwake kwa njia ya maandishi, kwa vile hawakujibiwa kwa wakati, hatimaye walalamikaji waliamua kwenda Wilayani kwa Mh. Mkuu wa Wilaya ili wasaidiwe kufikia ufumbuzi wa mgogoro huu.

4.2 Mlalamikaji wa 2 ndugu Damiani Mbiduka

Mwananchi huyu alieleza kuwa "eneo la mashamba yetu limechanganywa pamoja na eneo la VETA na HADO bila sisi wenyeji kushirikishwa, "aliendelea kutoa maelezo kuwa awali eneo la VETA lilikuwa ni shamba la kijiji, hata hivyo kuna wakati shughuli za kilimo za kijiji zilizorota hivyo shamba liliachwa bila kulimwa. Baadae Serikali ilileta Mpango wa Hifadhi ya Mazingira uliojulikana kama HADO. Kijiji kiliamua kurudi katika eneo lake ambalo awali lilikuwa shamba la kijiji na kuanza kupanda miti. Alihitimisha kutoa maelezo kuwa yeye mwenyewe alianza kulima shamba lake mwaka 1985.

4.3 MAELEZO YA SERIKALI YA KIJIJI CHA KIBAKWE

Ndugu Mario Mnyanju – mjumbe wa Serikali ya kijiji cha Kibakwe

Mjumbe huyu alitoa maelezo kama ifuatavyo;

" Sisi kama kijiji cha Kibakwe tulipewa taarifa za kutenga eneo la VETA na uongozi wa Wilaya, tuliamua kushirikiana na kijiji cha Iyenge kutafuta eneo la ujenzi, kwa vile mpango wa ujenzi wa chuo hicho ulikuwa ni wa Kata, wenzetu walishauri eneo la HADO ambalo lipo katika kijiji cha Iyenge tutenge eneo la ujenzi wa

shule ya Kata. Baadae Iyenge walionesha mipaka ya HADO hivyo ilionekana eneo hilo linalimwa na wananchi wa kijiji cha Kibakwe. Awali wananchi wote waliokuwa wanalima eneo hilo waliondolewa lakini baadae walirudi na kuanza kulima. Baada ya kukubaliana kutenga eneo la VETA hapo, kijiji cha Iyenge walitutaka tuwajulishe wananchi wetu wasiendelee kulima katika ardhi hiyo. Pia ilionekana baadhi ya wananchi wa Iyenge wanalima katika eneo hilo."

4.4 Maelezo ya mwananchi Gabriel Ngweitanile

Mwananchi huyu ambaye pia ni mstaafu aliyewahi kuwa mtumishi wa Umma, alitoa maelezo kuwa "*mimi niliwahi kulima katika huko 5 years before we were stopped, baadae niliitwa na kijiji na kuelezwa kuwa eneo hilo ni la HADO, Mipaka ya HADO ilivyowekwa hatukushirikishwa tulikuwa tunaambiwa tu ondoka kwa ajili ya HADO."*

4.5 MAELEZO YA AFISA TARAFA

Afisa Tarafa wa Tarafa wa kibakwe alitoa maelezo kama ifuatavyo;

"*Wamiliki wote wa eneo liliotengwa kwa matumizi ya VETA walishirikishwa kuoneshwa mipaka, pia awali eneo hilo lilikuwa la HADO, shughuli za hifadhi ya mazingira zililegalega, wananchi wakarudi kwenye maeneo hayo, kwa sasa Serikali imechukuwa tena maeneo yake ili yatumike kwa ujenzi wa chuo cha ufundi cha VETA. Pia niliwahi kuwapa walalamikaji ufafanuzi huu lakini walionekana kutoridhika hivyo nikawaelekeza kama hawajaridhika wasonge ngazi za juu*".

4.6 KUTEMBELEA ENEO LA MGOGORO

Baada ya kikosi kazi na watalaam kupokea maelezo ya mgogoro kutoka pande zote, kwa pamoja ilikubaliwa kuwa, pande hizo pamoja na watalaam wafike eneo la mgogoro.

Katika eneo la mgogoro wananchi hao wanne, kila mmoja alionesha mipaka ya eneo lake lilivyokaa, watalaam walichukuwa vipimo vya ardhini (coordinates) vya shamba la kila mwananchi na eneo lote la VETA. Kutokana na uhakiki wa ardhini ilibainika kuwa eneo lote la VETA lina ukubwa wa ekari 51.38 na mashamba ya walalamikaji yana ukubwa wa ekari 10.81. Eneo lisilokuwa na mgogoro lina ukubwa wa meta za eneo 40.57 (**Tazama Kiambatisho Na. 1).**

5.0 KILICHOBAINIKA

- Pande zenye mgogoro hazikubaliani mpaka wa eneo la VETA na Mashamba ya walalamikaji.
- Wakati wananchi wanne wamekatazwa na Serikali ya kijiji kulima katika eneo hilo, baadhi ya wananchi wengine wanaendelea kulima upande wa kasikazini wa eneo la VETA.
- Eneo lote la mashamba na VETA lina uoto wa asili unaofanana, yaani mibuyu mikubwa.
- Eneo la mgogoro ni ardhi ya kijiji cha Iyenge, wanaolima ni wakazi wa kijiji cha Kibakwe.
- Eneo la mgogoro lina ukubwa wa ekari 10.81 eneo lote la VETA ni ekari 51.38

6.0 USHAURI WA KITALAAM

- **Utengaji na upangaji wa ardhi unaofanywa na vijiji uheshimiwe**.

  Kwa vile Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999, Kifungu cha (8) kifungu kidogo (1) – (8)huelekeza kuwa Halmashauri ya kijiji ndiyo chombo pekee cha kusimamia maslahi ya ardhi katika kijijiji na kuridhiwa na Mkutano mkuu wa Kijiji, zoezi la utengaji wa eneo hili kwa matumizi ya umma liheshimiwe na kulindwa

kwa vile liliasisiwa n Serikali za vijiji vya Iyenge na Kibakwe na hatimaye kuridhiwa na vijiji, Kata, Tarafa na Wilaya.

- Wananchi wote wanaolima eneo la VETA wajulishwe kulima msimu huu, msimu unaofuata wasilime tena, eneo libaki wazi kwa matumizi ya umma.
- Eneo lote la VETA lipimwe na kuwekwa alama za kudumu (beacons) za upimaji ili kuzuia uvamizi kwa siku za baadae.

Tunaomba kuwasilisha;

Anderson Samson Mwamengo

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

MPWAPWA